**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**
**BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**

# TANGAZO LA MAFUNZO KWA WAENDESHA GHALA NA WAKAGUZI WA GHALA MSIMU WA ZAO LA KOROSHO 2025/2026

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Sura ya 339. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu cha 5 cha Sheria ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Bodi inapenda kuwajulisha waombaji leseni na wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuwa itaendesha mafunzo ya Wakaguzi wa Ghala na Waendesha Ghala. Mafunzo yanatarajiwa kuanza Tarehe **24 hadi 27 Septemba 2025** katika Chuo cha "**Stella Maris Mtwara University College"** kilichopo Mkoani Mtwara. Mafunzo haya yanalenga wadau wote wenye nia ya kufanya kazi kwenye Ghala Kuu za mnada kwa Msimu wa Korosho wa mwaka 2025/2026.

Gharama ya mafunzo pamoja na cheti kwa wataalam wapya ni **Shilingi laki saba na hamsini elfu tu (750,000**/=). Gharama hiyo itajumuisha Chai, Chakula cha mchana, Shajala na Cheti kwa watakaofaulu mtihani wa Bodi.

Aidha Mameneja wote wa Ghala zitakazotumika Msimu wa Korosho wa mwaka 2025/2026 wanawajibika kuhudhuria bila kukukosa siku ya **Tarehe 27/09/2025** kwa ajili na kupata taarifa mpya (Updates) za mfumo na maelekezo maalum kuelekea Msimu wa Korosho wa 2025/2026 kwa Gharama ya **Shilingi 100,000/=** kwa kila Mmoja. Mtaalam yeyote ambaye hatohudhuria mafunzo haya hataruhusiwa kufanya kazi katika Ghala Kuu la mnada.

Mwisho wa kufanya malipo ya mafunzo ni **Tarehe 19 Septemba, 2025;** wasiofanya malipo kwa muda huo hawatapokelewa.

Kwa maelezo zaidi na kupatiwa Namba ya malipo (*Control No.)* tafadhali wasiliana na **Bi Yasira Amir** kwa simu namba **0754897780** au **Bwana Omar Mafita** kwa simu namba **0756630180.**

**NB:** Kila Mshiriki wa mafunzo haya ni vyema kuja na kompyuta mpakato (*Laptop*) kwa ajili ya kujifunzia.

Imetolewa na
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala**
**11 Septemba 2025**